



Kongamano la
Kiswahili
Bayreuth



UNIVERSITÄT
BAYREUTH

Kongamano la Ishirini na Tisa la Kiswahili Bayreuth

Iwalewahaus, tarehe 6 Mei hadi tarehe 8 Mei 2016

Tarehe 4 Aprili 2016

Waalikwa Wapendwa – Mabibi na Mabwana,

Kwa mara nyingine tunawashukuruni sana kwa kuuitika mwito wetu. Kwa furaha tumepokea mihtasari na makala yenu. Kukutana nanyi nyote hapa kwetu itakuwa furaha hata zaidi. Karibuni sana!

Katika barua hii ya pili tunawatumia pia ratiba ya kongamano la mwaka huu, kama ilivyo kwa wakati huu. Kongamano la mwaka huu litafanyika *Iwalewahaus* – jumba la Taasisi ya Sanaa za Afrika ya Chuo Kikuu cha Bayreuth. Anwani ni: Iwalewahaus, Wölfelstr. 2, 95444 Bayreuth. Kongamano litaanza **Ijumaa tarehe 6**, saa mbili na nusu asubuhi. Kujisajili kutagharimu Euro 15 kwa wasio wanafunzi / Euro 10 kwa wanafunzi wageni.

Siku moja kabla ya Kongamano, yaani **Alhamisi tarehe 5**, tutakutana kwa chakula cha jioni kama ilivyo kawaida yetu. Mkahawa unaitwa 'Hua Hin' (Ludwigstrasse 30, 95444 Bayreuth). Tafadhali uelewe kwamba hatuwezi kulipa siku hiyo.

Bali na hayo kongamano letu lina mambo ya zaida: **Ijumaa** alasiri, Serena Talento (Chuo Kikuu cha Bayreuth) ataandaa meza duara inayohusu ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, ili walimu wa Kiswahili wapate fursa ya kujadiliana kuhusu changamoto za kufundisha Kiswahili na mbinu zake. Ijumaa jioni, kitabu kipya kinachohaririwa na Rose-Marie Beck na Kai Kresse chenye anwani "Abdilatif Abdalla. Poet in Politics" kitazunduliwa. Baadaye tutaonyesha filamu "Maisha, Maisha tu" na Yann Labry na Jakob Zeyer (Chuo Kikuu cha Leipzig).

Jumamosi jioni, kutakuwa na kiburudisho na mwanamuziki kutoka Zanzibar, Yahya Mbarak Harith atapiga muziki pia. Halafu Nathalie Koenings atasoma kutoka tafsiri yake ya *Vipuli vya Figo*. Mwishowe, ni furaha yetu kubwa ya kuwakaribisha washindi wa kwanza wa tuzo la Mabati-Cornell (Mabati Cornell Kiswahili Prize for African Literature). Kwa upande wa riwaya, Anna Samwel atasoma kutoka riwaya yake *Penzi la Damu* na kwa upande wa ushairi, Mohammed K. Ghassani atasoma baadhi ya mashairi kutoka diwani yake *N'na Kwetu*. Tuzo la

Mabati-Cornell ni tuzo la kwanza la fasihi lililowahusu waandishi wanaoandika kwa lugha za kiafrika (<http://kiswahiliprize.cornell.edu/>).

Kama una maswali yoyote ya zaida, usisite kuwasiliana nasi. Anwani ni: swahili@uni-bayreuth.de

Karibuni sana!

Salamu nyingi,

Ni sisi wenyeji wenu,

Clarissa Vierke, Nikitta Adjirakor na Serena Talento

Universität Bayreuth

Literaturen in afrikanischen Sprachen (GW I, Raum: 1.10)

95440 Bayreuth

Telefon: + 49 921 55-3550

Fax: + 49 921 55-3641

swahili@uni-bayreuth.de

http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/index.html